KUJIUNGA NA MPANGO WA SAGCOT

Mpango wa SAGCOT ni nini?

Mpango wa SAGCOT ni ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ulioanzishwa kwa lengo la kuendeleza kilimo cha kibiashara, na kuchochea mapinduzi katika kilimo kwenye Nyanda za Juu za Kusini mwa Tanzania. Programu hii hasa inalenga kuendeleza wakulima wadogo kusudi shughuli za uzalishaji kwenye mlolongo / mnyororo wa thamani zilete faida inayotarajiwa.

Kituo cha SAGCOT - ***SAGCOT Center Ltd*** ni kitovu cha ushauri mbalimbali wa kitaalam wa kilimo na pia ni kichocheo cha ushirikiano miongoni mwa asasi wabia zilizosajiliwa ili kuingiza mipango inayojumuisha minyororo ya thamani endelevu na yenye tija kwenye Kilimo.

Ifikapo mwaka 2030, wabia wa SAGCOT wameazimia kuboresha na kutumia hekta 350,000 za ardhi kwa uzalishaji wenye faida, kuwawezesha wakulima wadogo 100,000 kuanzisha na kuendesha kilimo cha biashara, kutengeneza fursa mpya za ajira 420,000, kuwainua watu milioni 2 kutoka kwenye umaskini, na kuzalisha dola za kimarekani bilioni 1.2 kama mapato ya kila mwaka ya kilimo.

"Ni wajibu wetu kuendeleza kilimo cha biashara kwa kutengeneza fursa zinazoongeza kipato kwa wakulima wadogo na kusimamia vizuri mali asili zilizopo. Kama Serikali tunakaribisha wabia wa uwekezaji ambao wako tayari kuchangia uwekezaji shirikishi na endelevu unaozingatia kanuni za mpango wa SAGCOT" – Mh. Christopher Chiza, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika katika Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Muundo wa SAGCOT

SAGCOT imeundwa na asasi wabia zilizosajiliwa ambazo ni mashirika/idara/ wakala mbalimbali wa serikali, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, taasisi za utafiti, wahisani, asasi za kiraia na vikundi vya wakulima.

Wadau wetu wa utaalamu mpana zaidi katika mnyororo mzima wa thamani kwenye kilimo, ambapo hubadilishana uzoefu mbalimbali katika utafiti, teknolojia, fedha, na biashara.

Muundo wa SAGCOT



FAIDA za kujiunga na mpango wa SAGCOT

Kuongeza Maarifa & kupanua Uhusiano

- Kushiriki katika mkutano mkuu wa mwaka - ***Annual SAGCOT Forum;*** fursa ya kubadilishana uzoefu na kutumia ya mbinu bora za uzalishaji
- Kuendeleza mtandao wako na kujenga uhusiano na wadau husika
- Kupata urahisi katika kuwafikia/kuwasiliana na wadau/watendaji wa umma na binafsi

Fursa za Mradi & Uraghbishi (Utetezi)

- Kukuunganisha na kushirikiana na wadau wengine wenye uwezo katika fikra ya uwekezaji na kubuni mradi
- Kushiriki kwenye mikutano, kazi mahsusi, na ziara katika sehemu za uzalishaji wa kilimo ili kubaini fursa zilizopo kwenye uwekezaji na mradi
- Kushiriki katika uraghbishi/utetezi juu ya vikwazo mbalimbali vya mradi na masuala ya sera kwa ujumla

MCHAKATO wa kujiunga na mpango wa SAGCOT

Kituo cha SAGCOT–SAGCOT Centre Ltd kinasaidia wabia katika kuendeleza minyororo ya thamani kwa pamoja. Wabia wengi hujiunga na mpango wa SAGCOT kama wabia wa jumla kupeana habari na kuangalia uwezekano wa kushirikiana kwenye uwekezaji na jitihada za pamoja za mnyororo wa thamani kwenye Kilimo katika kanda. Wabia wa ***Letter Of Intent - LOI Partners*** wako tayari kushirikiana katika uwekezaji maalum, miradi na malengo yake kwa kusaini randama za makubaliano.

Kwa kuongeza, Kituo cha SAGCOT kinatambua wabia mkakati watano hadi kumi kila mwaka ambapo:

- Kutoa ufumbuzi wa mwisho katika masuala ya mnyororo wa thamani na uwekezaji,
- Kuungana kwa wabia na kupanua ushirikiano,
- kutoa fursa katika kubaini au kuongeza matokeo chanya,
- kutoa matokeo ya mabadiliko kwa wakulima kwa usalama wa chakula na kuboresha maisha; na
- Umedhihirisha matokeo chanya ya uhifadhi wa mazingira.

Mchakato wa Ubia katika Mpango wa SAGCOT



Je, kituo cha SAGCOT kinaweza kufanya nini kwa Wabia?

Ikiwa wewe ni **mwekezaji uliopo,** sisi...

- Kuwa jukwaa la uwekezaji wa pamoja na wa kijani
- kuongeza fursa za uwekezaji, mitandao na ujuzi wa matumizi ya mbinu bora; na
- Kuweka angalizo katika vikwazo muhimu vya kisera kwa serikali ya Tanzania na taasisi husika.

Ikiwa wewe ni **mwekezaji mpya au mwenye uwezo,** sisi...

- Kukupatia habari na fursa ya kujiongezea maarifa,
- kutambua fursa mpya za uwekezaji na wabia; na
- kukutambulisha kwa mamlaka husika ya serikali.

Ikiwa wewe ni **asasi/kikundi cha wakulima,** sisi ...

- Kuongeza uhusiano katika minyororo ya thamani kwenye biashara na fursa za soko kwa wabia,
- kuwezesha miradi ambayo inatoa fursa kwa wakulimaili kuboresha upatikanaji wa pembejeo bora, teknolojia, na matumizi ya mbinu za Kilimo,na
- Huchangia kuboresha kipato na hali ya maisha kwa wabia

Ikiwa wewe ni **mshirika wa maendeleo au asasi ya kiraia,** sisi....

- kuunganisha shughuli kwenye miradi muhimu ya pamoja na endelevu, ili kuongeza kiwango cha matokeo yaletwayo uwekezaji wako,
- Kutoa fursa ya kuwepo ubora na ufanisi katika mfano wa maendeleo ya kilimo kwa kuzingatia uwekezaji binafsi; na
- kutoa fursa ya kushughulikia masuala muhimu ya kisera ya kubadilisha mfumo mzima wa Kilimo nchini

MISINGI YA UBIA katika Mpango wa SAGCOT

Kila mbia wa SAGCOT anapaswa kufanya yafuatayo...

- kushirikiana na wakulima wadogo na kuhakikisha uhifadhi endelevu wa mazingira wakati wa utekelezaji wa pamoja wa shughuli za kilimo,
- kushirikiana na wadau wengine kukuza mbinu unganishi na kuboresha ushirikiano,
- kudumisha ushirikiano, mawasiliano, na usaidizi kwa Kituo cha SAGCOT,
- kuchangia kwenye azimio la kuondoa vikwazo vya sera na miundombinu;
- Kuzingatia kwa kufuata taratibu mpya na zenye ubunifu za kifedha.

Unadhani kuna MASLAHI yoyote kwa mbia wa Mpango wa SAGCOT?

Kuzungumza na sisi.
Tunataka kujua zaidi kuhusu maslahi yako, shughuli zako, mawazo yako pamoja na rasilimali ulizonazo kuchangia kwenye ubia wa mpango SAGCOT.

Jaza fomu ya maombi.
Wafanyakazi wetu wanaweza kukupa nyaraka sahihi.

Andaa mpango.
Shirikiana nasi katika kuandaa mpango wenye malengo yako, shughuli na matokeo unayotarajia katika kanda uliopo Mpango wa SAGCOT.

SAGCOT
SOUTHERN AGRICULTURAL GROWTH CORRIDOR OF TANZANIA

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia;

SAGCOT Centre Limited
Tanzania Private Sector Foundation
(TPSF) Building
Plot No. 1288, Mwaya Road
Msasani Peninsula
P.O. Box 11313
Dar es Salaam, Tanzania

tel: +255 (0) 22 260 1024
+255 (0) 22 260 0146
fax: +255 (0) 22 260 2368

info@sagcot.com
www.sagcot.com

Uchapishaji wa kijarida hiki umewezeshwa na Serikali ya Tanzania, Shirika la Misaada la Uingereza (UK Aid), Shrika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID), Ofisi ya Ubalozi wa Norway-Tanzania na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Maneno yaliyomo katika kijarida hiki ni kazi iliyoandaliwa na Kituo cha SAGCOT-SAGCOT Centre Ltd na hayahusiani au kuakisi mawazo na mitazamo ya wahisani.

UKaid from the British people · USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE · World Bank Group Agriculture · NORWEGIAN EMBASSY · UNDP · AGRA Growing Africa's Agriculture

Kituo cha SAGCOT - SAGCOT Centre kinatoa shukrani za dhati kwa wabia wote kwa msaada wao wa hali mali katika kufanikisha kazi zetu.
Kupata orodha kamili ya wabia, tafadhali tembelea tovuti hii: **http://www.sagcot.com**